



**NAETISL**

National Association of  
Educational Translators and  
Interpreters of Spoken  
Languages



**MODDC**

Missouri  
Developmental  
Disabilities Council

# KUELEWA MIPANGO YA KUIINGILIA TABIA: MWONGOZO WA MZAZI

Ufadhili wa Mradi wa Kusaidia Ufikiaji wa Lugha Shuleni huko Missouri uliotolewa na Baraza la Walemavu wa Kiendelezi la Missouri, uliungwa mkono na Utawala wa Kuishi kwa Jamii (ACL), Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Marekani (HHS) kama sehemu ya tuzo ya usaidizi wa kifedha ya jumla ya \$1,361,246 na ufadhili wa asilimia 100 na ACL/HHS. Yaliyomo ni maelezo ya mwandishi na si lazima yawakilishe maoni rasmi ya, au uidhinishaji, na ACL/HHS, au serikali ya Marekani.



[naetisl@gmail.com](mailto:naetisl@gmail.com)

NAETISL



Follow us



MODDC



[moddc@moddcouncil.org](mailto:moddc@moddcouncil.org)



[www.naetisl.org](http://www.naetisl.org)

[www.moddcouncil.org](http://www.moddcouncil.org)





## **Mpango wa Kuingilia Tabia ni nini?**

Mpango wa Kuingilia Kati, kwa ufupi BIP, ni mpango ulioandikwa kwa lengo la kumsaidia mwanafunzi kubadilisha tabia zenye changamoto na zile chanya. Mpango huo una mikakati, usaidizi na uingiliaji kati ambao walimu na wafanyakazi watatumia kumsaidia mtoto wako kufaulu shuleni. Mpango huo pia unaweza kujumuisha mikakati ambayo unaweza kutumia nyumbani kumsaidia mtoto wako.

## **Je, kila mwanafunzi anayepokea huduma za elimu maalum huwa na BIP?**

Hapana, Mipango ya BIP huundwa kwa ajili ya wanafunzi binafsi ambao wanaweza kufaidika nayo. BIP pia zinaweza kutayarishwa kwa wanafunzi ambao hawapati huduma za elimu maalum.

## **Mtoto wangu anaweza kuhitaji mpango wa BIP kwa nini?**

Mpango wa BIP huundwa wakati tabia ya mwanafunzi inatatiza ujifunzaji wao au ujifunzaji wa wanafunzi wengine na haijaimarika kwa kutumia usaidizi wa kawaida.

Kwa mfano, mpango wa BIP unaweza kumfaidi mwanafunzi anayekataa kukamilisha kazi ya shule kila siku, au mwanafunzi anayejaribu kutoka darasani au shuleni mara kwa mara bila ruhusa.

## **Tofauti kati ya mpango wa BIP na sheria za kawaida za darasani ni gani?**

Ingawa sheria za darasani zinatumiwa kwa wanafunzi wote, BIP ni ya mtu binafsi. Imeundwa kulingana na mahitaji maalum ya mwanafunzi na sababu za tabia zao. Inatoa usaidizi uliolengwa kumsaidia mwanafunzi kujifunza tabia mbadala, zinazofaa zaidi.





## BIP hutengenezwa na nani?

Mwanafunzi akipokea huduma za elimu maalum, timu ya IEP hutengeneza BIP. Kulingana na hali, BIP inaweza kuandikwa wakati wa mkutano wa kila mwaka wa IEP au kuongezwa kwa IEP. Wazazi ni sehemu ya timu ya IEP na wanahitaji kujumuishwa katika mchakato huu.

Ikiwa mwanafunzi hapati huduma za elimu maalum, Timu ya Usaidizi ya Wanafunzi kwa kawaida hutengeneza mpango.

## Mpango wa BIP huundwa aje?

Kabla ya kuandika Mpango wa BIP, shule hufanya tathmini ya Tabia ya Utendaji (FBA).

Tathmini hii husaidia kutambua:

- Jinsi tabia ilivyo
- Lini na wapi ilifanyika
- Kwanini inafanyika (sababu- kama kuepuka kazi, kupata uangalifu, au mahitaji ya kihisia).

Kwa hivyo BIP inaundwa kulingana na matokeo ya tathmini ya FBA na inajumuisha mikakati ya kuzuia, kufundisha ujuzi mpya, na mbinu chanya za kuimarisha.





## BIP ya kina inajumuisha nini?

BIP iliyoundwa vizuri inafaa:

- Kueleza tabia iliyolengwa vizuri (ni tabia gani inayohitaji kupunguzwa au kubadilishwa)
- Kutambua hali zinazosababisha tabia fulani (vitu ama hali zinazosababisha au kuendeleza tabia)
- Kuorodhesha mikakati ya kuzuia tabia mbaya
- Kufunza mbinu za kubadilisha au kukabiliana
- Kujumuisha zawadi au uimarisho wa tabia nzuri
- Kueleza jinsi wafanyikazi wanafaa kujibu wakati tabia za matatizo zinapojitokeza
- Kueleza jinsi maendeleo yatakavyopimwa na kupitiliwa

## Nawezaje kuunga mkono BIP pale nyumbani?

Unaweza:

- Kutumia lugha thabiti na matarajio nyumbani na shuleni
- Kuwasiliana mara kwa mara na mwalimu wa mtoto wako kuhusu kinachofanya kazi
- Kuimarisha tabia nzuri katika taratibu za kila siku
- Kusherehekea maendeleo madogo— uthabiti na kutia moyo ni muhimu

## Nitajuaje BIP inafanya kazi?

Unafaa kupokea masasisho kupitia ripoti za maendeleo, mikutano, au mawasiliano ya kila siku. Ikiwa tabia inazidi kuboreka, mpango unaweza kubadilishwa kulenga maendeleo. Iwapo hakuna mabadiliko, timu itapitilia matokeo na kubadili mpango inavyohitajika.





## Iwapo sikubaliani na BIP au kufikiria kuwa haifai?

Una haki ya kuomba mkutano na timu wakati wowote kupitilia tena au kubadilisha mpango. Unaweza:

- Kuomba mapitio ya matokeo
- Kuomba usaidizi zaidi au masasisho ya mikakati
- Kushiriki kinachofanya kazi (au kisichofanya kazi) pale nyumbani.

